

JINA..... NAMBARI YAKO.....  
TAREHE.....

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

LUGHA

Julai/Agosti 2014

MUDA: SAA 2  $\frac{1}{2}$

**MTIHANI YA MAKADIRIO WA WILAYA YA GATUNDU**

**CHETI CHA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI**

KISWAHILI

Karatasi ya 2

LUGHA

Muda: saa 2  $\frac{1}{2}$

**MAAGIZO**

- \* Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ilioachwa hapo juu.
- \* Jibu maswali yote.
- \* Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.
- \* Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.
- \* Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

**Kwa Matumizi Ya Mtahini Pekee**

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
	80	

## 1. UFAHAMU

### Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Wahenga walisema “ntoto umleavyo ndivyo akuavyo.” Hii ina maana ya kuwa ukiogopa kutumia ufito kumchapa mtoto wako, ukamdekeza, atadeka na hatimaye ataharibika. Methali hii ina pacha yake ambayo ni, “Ukicha mwana kulia, utalia wewe.”

Hizi ni methali zilizoja busara kubwa. Mathalani, wewe ni mzazi au mtu ye yote mzima aliyetumikiwa madaraka juu ya watoto, lakini kila wanapokiuka uadilifu au mmoja wao anapokosea wewe unambembelez tu, basi huwa unaizorotesha tabia yake. Mwisho, mtoto huyo anaweza kuishia kuwa mtundi.

Hata hivyo, ni sharti tujue ya kwamba tuko katika njia panda hapa. Kwa upande mmoja, zamani ilichukuliwa kwamba watoto na hata wanawake watu wazima hawana akili. Kwa ajili hiyo, iwapo mwahamume mtu mzima ana jambo la kuwaeleza, njia pekee ya kuliingiza katika ‘akili’ yao “hafifu” ni kuwatwanga ili kulikongomeza jambo hili. Ukweli ni kwamba akili ya mtoto si hafifu hata. Unaweza kusema ni kama mmea, ambao “usiporutubishwa kimakusudi, ukapaliliwa vyema na kustawishwa stahiki yake, basi hudhoofu” na mwishowe kufifia.

Kwa upande mwingine, mtazamo wa kisasa ni tofauti kabisa. Imethibitishwa ya kwamba wanawake ni sawa kabisa katika maumbile yao wakilinganishwa na wanaume. Kwa jinsi hiyo, kweli wapo wanawake ambao hawana mwelekeo timamu kuhusu maisha, lakini ni kweli pia kuwa wapo wanaume watu wazima mamilioni ambao hawana akili. Kadhalika, si kweli kuwa watoto wote, kwa sababu ya umri wao tu, basi hawana akili. Ama kwa kusema kweli binadamu ye yote huzaliwa na akili zake timamu isipokuwa wale ambao kwa bahati mbaya maumbile yame wapa akili pungufu. Hili litokeapo, basi tunalikubali tu. Hatuwezi kumlaumu mtu kama huyo au muumba wake. Kwa hakika huu ndio msingi wa methali, “Akili ni nywele, kila mtu ana zake. “Vinginevyo, mtazamo wa kizamani ni taasubi kongwe tu za kiume zilizopitwa na wakati.

Aidha, kwa sababu watu wote huzaliwa na akili timamu, tena hawawi watu wazima kabla ya kuwa watoto kwanza, mtu mzima ye yote ana hali gani ya kuwadhulumu watoto na kujipambaniza na lawama za uongo dhidi ya vijana hao kwa madai kuwa hawana akili? Na je, ikiwa hawana akili, basi ndipo waonewe? Wanyanyaswe? Hili si jambo la busara. Kurudi mtoto kwa visa vya maonevu ni kumrudisha nyuma kiumbe huyo. Kurudi kufaako ni kwa kupeleka mbele, sio kwa kurudisha nyuma. Kurudi kuelekezako mbele ni kwa uongozi mwafaka, uongozi ambao lengo lake ni kummilikia mtoto kurunzi ilimradi kumwangazia tarika njema

Mtoto asinyimwe vya tunu vyovoyote ambavyo ni stahiki yake, kwa kisingizio kuwa vimetengewa mtu mzima, ndugu mkubwa, mwalimu, au mtu awaye ye yote yule aliyekabidhiwa jukumu la kumlea au kumwongoza mtoto.

Mtoto ana haki ya kuhudumiwa kwa njia yoyote ifaayo ili akue na akili yake ikomae kikamilifu. Inafaa asomeshwe, apewe malezi bora ili naye aje ale wengine kistahiki.

### Maswali

- a) “Mapenzi yasiyo kipimo yanaweza kuwa hatari kwa mtoto” Eleza kikamilifu huku ukirejelea habari uliyosoma. (alama 2)

- b) Fafanua njia panda inayorejelewa na mtunzi. (alama 2)

.....  
.....  
.....

- c) Mtoto analinganisha na mmea katika taarifa hii, kwamba “Usiporutubishwa kimaksudi, ukapaliliwa vyema na kustawishwa stahiki yake, basi hudhoofika.” Tathmini. (alama 4)

.....  
.....  
.....  
.....

- d) “Akili ni nywele, kila mtu ana zake.” Eleza maana ya ndani ya methali hii kulingana na taarifa. (alama 2)

.....  
.....  
.....

- e) Onyesha kwamba unaelewa maana ya:

“Kurudi mtoto kwa visa vya maonevu ni kumrudisha nyuma kiumbe huyo”. (alama 3)

.....  
.....  
.....  
.....

- f) Eleza maana ya: (alama 2)

- a. Kilikongomeza

.....  
.....  
.....

- b. Kujipambaniza

.....  
.....  
.....

## Muhtasari

### Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Kuna fikra inayotawala siku hizi kuwa jela si mahali pa adhabu bali matibabu. Yaani lengo la kumfunga mhalifu si kumuadhibu bali kumtibu kwa njia ya kurekebisha tabia ili aweze kuchangia katika maendeleo ya jamii yake anapoachiliwa.

Wataalamu wa masuala ya urekebishi tabia wanasema kuwa mhalifu akiadhibiwa sana na kufanyishwa kazi ngumu anapokuwa kifungoni, huishi kuwa sugu zaidi kuliko alipofungwa. Kwa hivyo, Wataalamu wanasisitiza umuhimu wa kutilia mkazo lengo la kumtia mtu jela kuwa ni kumjenga kitabia. Mijizi, minyag'anystha wauaji wanapotoka gerezani kama hawakubadilishwa hurejelea tabia zao na kuhatarisha zaidi maisha ya watu wengi.

Ajabu na kinaya ni kwamba baadhi ya wahalifu nchini na kwingineko wametokea kupata faida kuu kutokana na vifungo vyao. Kuna wafungwa ambao wamewahi kuandika hadithi za kusisimua kuhusu maisha yao na kutokea kuwa mabilionea. Magazeti na vyombo vya habari pia huvutiwa na habari kuhusu maisha yao. Mara kwa mara, magazeti hujaa habari kuhusu mambo kama haya. Pia kuna sinema nyingi ambazo zimetungwa kufuata maisha ya wahalifu Fulani.

Watetezi wa haki za kibinadamu wanadai kuwa yale wafungwa walikuwa wakitendewa, na bado wanatendewa katika nchi nyingine, ni kinyume na haki za kimsingi za binadamu. Hali hii imepelekea magereza mengi kukarabatiwa ili kuweza kukidhi mahitaji ya "ubinadamu".

Nchini Kenya, wafungwa sasa wameanza kushughulikiwa kwa kila hali. Sikwambii wanapata chakula kizuri chenyе viinileshe bora, malazi bora, maji safi na mazingira nadhifu kwa jumla. Kumeanzishwa pia mpango wa elimu ambao ni maalumu kwa wafungwa magerezani. Sasa wafungwa wanapata elimu na kuhudhuria madarasa na hata kuufanya mtihani wa kitaifa. Vilevile magereza nchini yameanzisha pia mpango wa kuwa na mashindano ya kila aina ya kati ya magereza mbalimbali. Kuna mashindano ya michezo mathalan kandanda, voliboli, na michezo mingine na juu ya yote, maajuzi magereza yalianzisha mashindano ya urembo baina ya wafungwa wa kike.

Kilele cha kuboreshwa kwa hali za magereza nchini Kenya ni kuanzishwa kwa huduma za kuwastarehesha wafungwa hao. Sasa wafungwa wa humu nchini wanaweza kusoma magazeti na hata kutazama runingi ili kupata habari kuhusu yanayotendeka nchini wanapoendelea kutumikia vifungo vyao.

Hata ingawa serikali imeanzisha mpango hii ya kuboresha hali katika magereza ya Kenya, kuna matatizo mbalimbali ambayo yanaendelea kukumba taasisi hii. Kwanza, ni msongamano wa wafungwa uliopo. Magereza mengi yana wafungwa maradufu ikilinganishwa na idadi yanayofaa kuwa nayo. Hali hii imepelekea kuzuka kwa magonjwa na madhara ikilinganishwa na idadi yanayofaa kuwa nayo. Hali hii imepelekea kuzuka kwa magonjwa na madhara mengine. Hii imewafanya watetezi wa haki za kibinadamu kuitaka serikali ianzishe mpango wa kutoa vifungo vya nje kwa wahalifu wenyе makosa madogo madogo ili kuondoa msongamano huo.

## Maswali

- a) Kwa nini wataalamu na watetezi haki za binadamu wanapinga hali ya kuwaadhibu wafungwa? (maneno 20-30) ~~KCSAOP~~ (alama 5)

MATAYARISHO

A red watermark is positioned diagonally across the page. The text "IIT-JEE Past papers" is at the top left, and "Visit www.IIT-JEE-Past-Papers.com" is at the bottom right, separated by a small gap.

JIBU

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

- b) Eleza mabadiliko ambayo yamefanywa katika idara ya magereza nchini Kenya. (maneno 60-70)  
(alama 7)

MATAYARISHO

---

---

---

---

MATUMIZI YA LUGHA

- a) (i) Taja sauti ya king'ong'o cha kaakaa laini. (alama 1)

(ii) Andika sauti moja ya kipasuo kwamizo. (alama 1)

- b) Tumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari kuandika tena sentensi ifuatayo.  
Umoja wa jamii hiyo umewawezesha kupigana na umaskini (alama 2)

.....  
.....  
.....

- c) Eleza miundo ya silabi katika neno lifuatalo.  
Kichwa (alama 2)

.....  
.....  
.....

- d) Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mistari  
Yule mzembe alifika leo asubuhi (alama 2)

.....  
.....  
.....

- e) Ainisha shamirisho na chaagizo katika sentensi ifuatayo.  
Wakulima walifanya kazi haraka sana kwa jembe. (alama 3)

.....  
.....  
.....

- f) Tunga sentensi ukitumia kiunganishi cha kuleta dhana ya kujumuisha. (alama 1)

.....  
.....  
.....

- g) Ainisha vielezi vya namna katika sentensi ifuatayo.  
Wanafunzi waojikaza kisabuni hunyamaza jii darasani. (alama 2)

.....  
.....  
.....

- h) Tambua aina za nomino na utaje zimo katika ngeli zipi.  
Kuumia kwake kulisababishwa na kujikata kwa wembe. (alama 2)

.....  
.....  
.....

- i) Chorea sentensi ifuatayo kielelezo matawi  
Njoroge si intiifu ingawa yeye ni mwerevu sana, (alama 4)

For More Free KCSE Past papers Visit [www.FreeKCSEPastPapers.com](http://www.FreeKCSEPastPapers.com)

- j) Eleza matumizi ya “kwa” katika sentensi ifuatayo.

Walivuka barabara kwa haraka wakienda kwao na sita kwa kumi wakagongwa kwa gari.(alama 2)

.....  
.....  
.....

- k) Eleza maana mbili zinazojitokeza kwenye sentensi ifuatayo.

Walimwibia Juma baiskeli. (alama 2)

.....  
.....  
.....

- l) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi.  
Mwalimu alitaka kujua kama wanafunzi wangeenda kumuona siku hiyo. (alama 3)

.....  
.....

m) Kanusha

Wanafunzi watundu waliadhidiwa na kuaibishwa. (alama 2)

.....  
.....  
.....

n) Nyambua vitenzi vituatavyo katika kauli ulizopewa.

(alama 2)

a. Oa .....(tendesha)

b. Kokoa..... (tendata)

o) Tunga sentensi mojamoja kubainisha:

(alama 2)

a. Kiwakilishi cha pekee chenye maana ya umilikaji.

.....  
.....

b. Kiwakilishi cha nafsi kiambata.

.....  
.....

p) Andika kinyume;

Shangazi angeingia tungemsifu.

.....  
.....

(alama 2)

q) Tunga sentensi mojamoja kudhihirisha matumizi ya (alama 2)

a. “ka” ya mfululizo

.....  
.....

b. “a” isiyodhihirika

.....  
.....

r) Eleza matumizi mawili ya mabano.

(alama 2)

.....  
.....  
.....

- s) Onyesha kiima katika sentensi ifuatayo.  
Wachezaji hao walicheza vizuri wakashinda. (alamu 1)

*www*

#### 4. ISIMU JAMII

- a) Eleza sababu tano za watu kuchanganya ndimi au kubadili msimbo. (alama 5)

- b) Eleza umuhimu wa sajili za lugha. (alama 5)

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---